



COVID-19: Sheria mpya kwa watu wa nyumbani na watu wa karibu katika NSW

Ikiwa wewe ni mtu wa nyumbani au wa karibu na huna dalili zozote za COVID-19, huna haja ya kujitenga lakini lazima ufuate miongozo ya NSW Health:

- Usitembelee maeneo ya hatari kubwa kama vile hospitali na vituo vya huduma za wazee
- Fanya kazi au soma nyumbani inapowezekana. Unahitaji idhini kutoka mwajiri wako au kituo chako cha elimu kama unahitaji kwenda kazini au shuleni
- Vaa maski/barakoa ndani ya majengo ikiwa una umri wa miaka 12 na zaidi. Huna haja ya kuvaa maski nyumbani yako mwenyewe
- Epuka mikusanyiko mikubwa au msongomano ya ndani na watu ambao huishi nao. Ikiwa ukihitaaji kuhudhuria, fanya kipimo cha haraka cha antijeni kabla ya kwenda

Fuata sheria kwa siku 7 kuanzia mara ya mwisho ambapo mtu katika nyumba yako alipopata majibu chanya ya kupimwa kwa COVID-19.

Ikiwa unazo au ukipata dalili, lazima ujitenge na kupimwa kwa COVID-19. Fuata ushauri wa NSW Health kama jibu lako la kipimo ni chanya.

Ikiwa jibu lako la kipimo ni hasi, kaa nyumbani hadi hupati dalili zozote.

Tembelea www.nsw.gov.au/covid-19/management/household-contacts kwa habari zaidi.